JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI

S.L.P. 38 KYAKA - KAGERA

Kumb.Na.KGR/MSY/C.4/7/VOL.III/03 24 Oktoba, 2024

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi amepokea Kibali cha Ajira Mpya kutoka kwa Katibu Mkuu – ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia baru ayenye **Kumb. Na. FA.97/228/01/09** ya tarehe **25.06.2024.** Hivyo anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa za kujaza nafasi zifuatazo:-

## 1.0 DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 3)

### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe amehitimu Elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) awe na Lesseni ya Daraja la C au E ya uendeshaji wa magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.

ii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari **'Basic Driving Course"** yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA au NIT) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

iii. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

### 1.2 MAJUKUMU YA KAZI:-

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;

ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi;

iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari;

iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali;

v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari;

vi. Kufanya usafi wa gari;

vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

2.1. NGAZI YA MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara wa TGS B

3.0 <u>MSAIDIZI MAENDELEO YA JAMII DARAJA LA II (NAFASI 05)</u>

3.1 <u>SIFA ZA MWOMBAJI</u>

i. Awe amehitimu Elimu ya kidato cha nne (IV) au kidato cha (VI);

ii. Awe na Astashahada katika fani ya Maendeleo ya Jamii, Mipango na Usimamizi wa miradi na fani nyingine zinazofanana na Maendeleo ya Jamii kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

3.2 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kusadia kubuni na kupanga mipango na miradi ya maendeleo katika eneo lake;

ii. Kusaidia uwezeshaji na upatikanaji wa mafunzo kuhusu masuala ya maendeleo katika eneo lake;

iii. Kushiriki katika utekelezaji wa shughuliza maendeleo;

iv. Kusaidia kutoa elimu kuhusu kazi za kujitegemea katika eneo lake;

v. Kuandaa na kutoa taarifa za kazi za maendeleo ya jamii kila mwezi kwa uongozi wa kijiji na kwa Msimamizi wake wa kazi;

vi. Kusaidia kuunda vikundi vya kijamii na vya kimaendeleo;

vii. Kutambua na kuwezesha kaya masikini kuinua uchumi wao kupitia fursa na Rasilimali zinazowazunguka;

viii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

3.3 MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali TGS B.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

i. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45;

ii. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika;

iii. Mwombaji aambatishe cheti cha kuzaliwa kilichodhibitishwa na Mwanasheria/Wakili;

iv. Maombi yote yaambatane na cheti cha taaluma na nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika

- Certificates;
- Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI;
- Vyeti vya kitaaluma (professional Certificates)
- Picha moja 'pasport size' ya hivi karibuni;

v. Testimonials 'provisional results' results slip' kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa *HAVITAKUBALIWA.*

vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).

vii. Waombaji wa nafasi za ajira waliostaafishwa / kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi;

viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria;

ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.

x. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni *tarehe 06 November, 2024 saa 9: 30 alasiri.*

xi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **hayatafikiriwa;**

xii. Mwombaji atatakiwa kuambatisha nakala ya kitambulisho cha uraia (NIDA) au namba ya NIDA kama hana kitambulisho;

xiii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa Ajira ulemavu walionao;

xiv. Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi,
S.L.P 38,
KYAKA – MISSENYI

xv. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielectroniki wa Ajira Recruitment Portal kupitia anuani ifuatayo: https://portal.ajira.go.tz (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuto ya Seckretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal')

xvi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.

*LIMETOLEWA NA:*

John P Wanga
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI